# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 029 MEI 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 ELIMU YA HALI YA HEWA YATOLEWA KWA WATU WENYE UHITAJI MAALUM

## 2 TANZANIA YAPEWA KIPAUMBELE UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU YA HALI YA HEWA



## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2023



KITAIFA

# ELIMU YA HALI YA HEWA YATOLEWA KWA WATU WENYE UHITAJI MAALUM

**Pwani**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Walemavu Tanzania (SHIVYAWATA) iliwajengea uwezo watu wenye uhitaji maalumu kwa kutoa elimu ya masuala mbalimbali ya hali ya hewa ikiwemo uchambuzi wa hali ya hewa kuanzia ngazi ya uangazi hadi usambazaji, Elimu hii pia ilihusisha aina mbalimbali za utabiri wa hali ya hewa kuanzia utabiri wa muda mfupi, kati, mwezi, msimu, hali mbaya ya hewa na athari zake, mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi pamoja na majukumu ya Mamlaka, kupitia warsha iliyofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC), Ikwiriri, Rufiji.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Katibu wa SHIVYAWATA Rufiji Bwana Abdul Warusimbi aliishukuru TMA kwa kufika Ikwiriri na kuweza kutoa elimu ambayo itawasaidia katika kukabiliana na majanga yatokanayo na hali mbaya ya hewa kwa washiriki 100 kutoka Rufiji, Nyamisati na Visiwa vya Chole na Mafia.

“Katika siku za hivi karibuni kumetokea majanga mbalimbali ambayo yamesababishwa na mabadiliko ya hali mbaya ya hewa, majanga hayo yalikuwa yakiwaathiri watu wenye ulemavu kwa kiasi kikubwa hususan watu wa vijijini. Kupitia TMA walijifunza kuwa kila hatua ya maisha wanayopiga wanahitaji usaidizi wa

utabiri wa hali ya hewa". Alisema Abdul Warusimbi.

Kwa upande wake, Bwana. Haji Omari Mpili maarufu kama Mzee Mpili, alisema TMA ina wataalamu waliobobea katika masuala ya hali ya hewa na kuwataka wananchi wa Kusini kuacha kutumia utabiri wa kizamani wa kusoma nyota na kujikita katika utabiri wa kisayansi ambao unafanyiwa utafiti wa kitaalamu.

"Mfano hivi sasa msimu wa mvua umeisha lakini kuna watu wengine wanaendelea kupanda. Je, mimea hiyo itafanikiwa? taarifa za hali ya hewa kutoka TMA zinaeleza mvua itaanza kipindi gani na itamalizika kipindi gani, ni vizuri kufuatilia taarifa hizo zenye uhakika". Alisema Mzee Mpili.

Akizungumza mara baada ya mafunzo hayo, Bwana. Hassan Said Bakari, Mkuu wa Kituo cha Hali ya Hewa Kilwa Masoko, alisema utabiri wa msimu wa mvua ulitabiriwa kuwa chini ya wastani kwa maeneo ya Kusini mwa nchi na kuwataka wananchi kufuatilia taarifa za hali ya hewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

"Mamlaka ilipokea maoni mbalimbali yaliyotolewa na watu wenye uhitaji maalumu na kupitia maoni yao, TMA itayafanyia kazi ili kuhakikisha kundi hili maalum linafikiwa kwa urahisi, vilevile Mamlaka iliendelea kuwakumbuhsha kufuatilia taarifa za hali ya hewa zionazotolewa mara kwa mara ili kuweza kufanya uzalishaji wenye tija hususan kipindi hiki cha changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi". Alisema Bw. Bakari.

Bi. Nunu Salimu, mkazi na mkulima kutoka Ikwiriri alieleza namna ambavyo alitumia taarifa za hali ya hewa zilizitolewa mwezi Oktoba 2023 na kufanya maamuzi ya kutumia mbegu za muda mfupi, hivyo kufanikiwa kupata mavuno mengi wakati wakulima wengine wakipata hasara kutokana na kutumia mbegu za muda mrefu.



KIMATAIFA

# TANZANIA YAPEWA KIPAUMBELE UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU YA HALI YA HEWA

**Dodoma**



Tanzania kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Hali ya Hewa ya Denmark, zilikutana na wadau katika warsha maalumu ya kuangalia mapungufu ya nchi katika miundo mbinu ya hali ya hewa ili kuweza kufanya maboresho ambayo yatasaidia kuleta tija katika utoaji huduma za hali ya hewa kwa maendeleo ya Taifa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dkt. Ladislaus Chang'a alieleza kuwa Tanzania imepata fursa ya kuchaguliwa kuwa miongoni mwa nchi 26 duniani ambazo zimepewa kipaumbele katika kuimarisha huduma za hali ya hewa kupitia miundo mbinu ya uangazi wa hali ya hewa chini ya mwamvuli wa Mfuko wa Kuimarisha Uangazi wa hali ya hewa (Systematic Observations Financing facility-SOFF). Mfuko huu umekuwa ukichangiwa na nchi mbalimbali duniani, na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na Mpango wa Umoja wa Matatifa wa Kusaidia Maendeleo Duniani (UNDP).

Dkt. Chang'a alisema, "fursa hii ni muhimu kwa Tanzania hususan kipindi hiki ambacho dunia ikiwemo nchi yetu inakabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi, changamoto hizi zinahitaji msukumo wa kipekee katika kuimarisha miundombinu ya hali ya hewa

lakini vilevile, utoaji wa huduma hususan huduma za utabiri na tahadhari za hali mbaya ya hewa". Alisema Dkt. Chang'a.

"Hii ni mojawapo ya jitihada ambazo zinaenda kuchangia katika jitihada kubwa zinazofanywa na serikali yetu ya kuimarisha huduma za hali ya hewa na kuongeza uwezo wetu wa kuhimili changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa. Tunaishukuru sana Serikali". Aliongeza Dkt. Chang'a.

Kwa upande wake Bw. Christian Johansen, mwakilishi wa Taasisi ya Hali ya Hewa ya Denmark (DMI), alisema ushirikiano baina ya Tanzania na Denmark ni wa muda mrefu na unaendelea kukua. Ushirikiano wa sasa baina ya TMA, DMI na UNDP unalenga kuboresha huduma za hali ya hewa kwa kuimarisha miundombinu ya uangazi pamoja na kuendeleza mahusiano mazuri yaliyowekwa baina ya nchi hizi mbili. Alisema kupitia program ya SOFF waliweza kutembelea katika maeneo ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Mwanza na Tabora, na kufanya tathmini ya uwezo na mahitaji katika kuimarisha uangazi na kupitia warsha hii wanatarajia kupata taarifa zaidi za maeneo mengine ya nchi yanayohitaji maboresho na uimarishaji wa mfumo wa uangazi.

Naye mwakalishi mkazi wa UNDP Tanzania, Bi. Christine Musisi alishukuru kwa mahusiano mazuri baina ya UNDP na TMA, ikiwemo misaada mbalimbali ambayo UNDP imekuwa ikitoa kusaidia uimarishwaji wa huduma za hali ya hewa. Alieleza kuwa takwimu zinaonesha ongezeko la matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo matukio ya mafuriko, na hivyo programu hii itasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za hali ya hewa na za uhakika na hivyo kuchangia katika kuongeza kasi ya maendeleo katika sekta muhimu kama vile kilimo, mifugo, nishati, uchukuzi, afya na maji. Aidha, aliongeza kusema kuwa uboreshaji wa miundombinu ya hali ya hewa ni kwa manufaa ya nchi na dunia kwa ujumla.



JARIDA LA MWEZI

06 TOLEO NA. 029 MEI 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2023

Kipindi cha mwezi Juni 2023, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani. Hata hivyo, hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi hususan nyakati za usiku na asubuhi inatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na nyanda za juu Kusini magharibi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya upepo mkali vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 26 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya nyuzi joto 14 °C na 22 °C katika maeneo ya nchi kavu. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Juni.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. **Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 15 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 11 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 7 °C hadi 16 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 7 °C. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi. |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 12 katika kipindi cha mwezi Juni, 2023. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. |

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# BIDHAA NA HUDUMA ZA TMA

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA KWA WAENDESHAJI WA SIMU ZA MKONONI/SEKTA YA MAWASILIANO

TMA inatoa huduma za utabiri wa hali ya hewa mahususi kwa waendeshaji wa simu za mkononi kwenye sekta ya mawasiliano. Huduma hizi zinatolewa kwa kufuata na kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**TMA inatoa huduma zifuatazo kwa waendeshaji wa simu za mkononi**


(a) Taarifa za kihistoria za eneo za ya hali ya hewa kama vile joto, unyevuanga, mawimbi ziwani na baharini, kasi na mwelekeo wa upepo;
(b) Utabiri wa hali ya hewa;
(c) Utabiri wa hali mbaya ya hewa pamoja na Tsunami;
(d) Uono;
(e) Utabiri wa msimu kwa maeneo mahsusi

**Matumizi ya huduma za hali ya hewa zitolewazo na TMA katika shughuli za ujenzi**

(a) Ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano;
(b) Uboreshaji wa utendaji wa mtandao;
(c) Usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji mbalimbali;
(d) Matumizi mengine yanayohusiana










## JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Bakari Msambekwa
Monica Mutoni

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.